East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1271

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 1, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Maumbo na Maana za Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo

*Jemima Lenjima [1*] na Dkt. Julius Edmund Frank, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, S. L. P. 1100 – 20300 Nyahururu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: lenjimajemima7@gmail.com ORCID ID: https://orcid.org/0009-0009-5050-1739;

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1271**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*28 Juni 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Jina, Jamii-lugha, Maumbo ya Majina, Maana, Majina ya Asili.*

**IKISIRI**

Makala haya yamechunguza maumbo na maana za majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo kwa kuchanganua vijenzi mbalimbali vinavyojenga majina hayo. Data iliyochunguzwa ni sehemu ya data iliyokusanywa kutoka katika wilaya ya Mpwapwa na Chamwino, mkoani Dodoma kwa ajili ya tasnifu ya Uzamivu. Uchanganuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksika kwa mujibu wa Kiparsky (1982) inayosisitiza kuwa vipashio vinavyounda maneno vimepangwa kidarajia kimsonge ambapo vipashio vidogo huungana ili kuunda vipashio vikubwa. Data za makala haya zimewasilishwa kwa majedwali. Hata hivyo, baadhi ya data zimewasilishwa kwa kutumia michoroti ili kudadavua vyema mpangilio wa vipashio vinavyounda majina husika na kuonesha jinsi vipashio hivyo vilivyopangwa kidarajia kimsonge. Matokeo ya uchanganuzi huo yamedhihirisha kuwa majina ya asili ya watu yaliyochunguzwa yameundwa kwa vijenzi mbalimbali ambavyo vimechanganuliwa kimofolojia na kuleta maana. Tofauti na baadhi ya wanaisimu wanaodai kuwa majina ya watu yameundwa na mzizi au mashina tu, makala haya yamedhihirisha kuwa vipo vipashio maalumu vinayounda majina ya asili ya watu na vinaweza kuchanganuliwa kimofolojia.

**APA CITATION**

Lenjima, J. & Frank, J. E. (2023). Maumbo na Maana za Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 209-232. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1271.

**CHICAGO CITATION**

Lenjima, Jemima and Julius Edmund Frank. 2023. "Maumbo na Maana za Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 209-232. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1271.

**HARVARD CITATION**

Lenjima, J. & Frank, J. E. (2023) "Maumbo na Maana za Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 209-232. doi: 10.37284/jammk.6.1.1271.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1271

**IEEE CITATION**

J. Lenjima & J. E. Frank, "Maumbo na Maana za Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 209-232, Jun. 2023.

**MLA CITATION**

Lenjima, Jemima & Julius Edmund Frank. "Maumbo na Maana za Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Jun. 2023, pp. 209-232, doi:10.37284/jammk.6.1.1271.

## UTANGULIZI

Lugha mbalimbali duniani huwa na vijenzi maalumu vinavyounda maneno. Maneno huundwa kwa neno mojamoja bila kuchanganyika na viambishi. Katika lugha ambishi bainishi kama Kiswahili na Kigogo, maneno huundwa kwa mfuatano bayana wa mofimu. Mofimu hizo huwa na maana na mizizi hudhihirika wazi bila kuchanganyika na viambishi. Mofimu katika lugha ambishi changamani huwa na uamilifu zaidi ya moja.

Licha ya lugha za kibantu kama Kiswahili na Kigogo hutambulika kama lugha ambishi bainishi, majina ya watu yamekuwa yakitazamwa kama maneno yaliyoundwa kwa mofimu moja tu hivyo hakuna utafiti uliochunguza vijenzi vya majina ya watu hususani majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo. Ingawa kuna tafiti kadhaa zilizofanya ama kwa kushughulikia asili na maana za majina kama vile (Tegisi, 2019), (Anusa, 2016), (Zuber, 2015), (Abdul, 2013), (Manyasa, 2010) na (Baitani, 2010). Wamegusia baadhi ya vipengele vya majina ya watu. Hata hivyo, tafiti zilizofanywa zilifanya kuhusu majina ya watu zilishughulikia maana na vigezo vya uteuzi wa majina ya watu na kutoshughulikia vipengele vya kimofolojia vya majina ya watu. Inawezekana kuwa labda kutoshughulikiwa kwa vipengele hivyo ni kutokana na madai yaliyotolewa na baadhi ya wanaisimu kama vile (Agard, 1984) na (Habwe & Karanja, 2004) kuwa nomino mahususi huundwa na mzizi tu, hivyo haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia. Kutokana na madai hayo, makala haya yameangazia vijenzi mbalimbali vya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Sehemu hii imeshughulikia mapitio ya maandiko. Katika kipengele hiki tumepitia maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya makala haya. Maeneo yaliyopitiwa ni tafiti tangulizi zilizobainisha maumbo ya majina ya vitu na mahali pamoja na kutokuwepo kwa tafiti tangulizi zilizobainisha maumbo ya majina ya watu.

### Tafiti Zilizobainisha Maumbo ya Majina ya Vitu na Mahali

Utafiti wake Buberwa, (2017) ulichunguza ruwaza za kimofolojia za majina ya mahali ya Kihaya. Katika matokeo ya uchanganuzi wake majina ya mahali ya Kihaya yaliyochunguzwa yameundwa kwa vijenzi mbalimbali ambavyo vimechanganuliwa kimofolojia. Tofauti na madai ya baadhi ya wanaisimu kuwa majina ya mahali yameundwa na mizizi au mashina tu, utafiti huu umethibitisha kuwa vipo vipashio maalumu vinavyounda majina ya mahali na vinaweza kuchanganuliwa kimofolojia.

Davis (2016) ambaye utafiti wake ulilenga kubainisha majina ya asili ya vitongoji na kuchambua maumbo ya majina ya asili ya mahali ya vitongoji yanayoitambulisha jamii ya Wajita. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa kuna majina ya asili ya mahali ya vitongoji yanayobeba utambulisho wa jamii ya Wajita. Vile vile utafiti huu umebaini vigezo kumi na moja (11) vinavyotumika kutoa majina ya mahali ya vitongoji, vigezo hivyo vinazingatia kuwepo kwa mabonde ya maji, koo za watu, milima, makorongo, mawe au miamba, wanyama, miinuko ya ardhi, umaarufu wa watu, upekee wa miti, vichaka, misitu, na aina ya udongo. Aidha utafiti umedhihirisha majina ya mahali ya vitongoji yanatumia maumbo ya nya, ku, mwi, na bha katika kutambulisha majina ya mahali ya vitongoji katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

jamii ya Wajita.

Rugemalira, (2005) alichunguza majina ya mahali katika jamii ya Runyambo. Katika utafiti wake alichunguza mbinu za kimofolojia zinazotumika katika kuunda majina ya maeneo. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kwamba majina ya mahali katika jamii hiyo yanaundwa kwa kutumia utaratibu maalumu wa kimofolojia.

## MISINGI YA NADHARIA

Kipengele hiki kinahusiana na misingi ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti (metholodolojia) zilizotumika.

### Nadharia ya Mofolojia Leksika

Nadharia ya Mofolojia Leksika iliibuka kutokana na maoni ya (Pesetsky, 1976) na kufafanuliwa na (Kiparsky, 1982) pamoja na mikabala mbalimbali ambayo ni; Mkabala wa Mofolojia na Leksika (Aronoff, 1976); Mkabala wa Mofolojia Darajia (Siegal 1974,1977; Allen, 1978) na Mkabala wa Matatizo ya Kudhibiti Uwakilishi wa Kileksika na Kanuni za Kifonolojia (Kiparsky, 1968; Mascaro, 1976; Rubach, 1981) na (Kiparsky, 1982).

Nadharia ya Mofolojia Leksika ina mihimili mbalimbali ambayo ni pamoja na kanuni ya ngazi leksika, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya kufuta mabano, kanuni ya ufinyu wa sifa, kanuni ya kwingineko, na kanuni ya kuhifadhi muundo (Gichuru, 2010; Buberwa, 2017). Kutokana na mihimili hiyo, makala haya yamejihusisha na mhimili wa kanuni ya ngazi leksika ambayo ni darajia za uundaji wa maneno huunganishwa hatua kwa hatua na kujenga vipashio vikubwa zaidi. Darajia zilizohusishwa katika utafiti ni za (Kiparsky, 1982).

Baadhi ya watafiti tangulizi waliotumia nadharia ya Mofolojia Leksika ni (Buberwa, 2017) katika utafiti wake uliohusu Ruwaza za Kimofolojia za Majina ya Mahali ya Kihaya: Mtazamo wa Mofolojia Leksika. (Gichuru, 2010) utafiti wake ulihusu Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili Mtazamo wa Mofolojia Leksika.

Nadharia ya Mofolojia Leksika imetumika katika kuchunguza maumbo na maana za majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo ambacho ndicho kiini cha makala haya na kuonesha namna viambishi vyenye sifa vinavyochopekwa katika neno, shina na mizizi yenye kuunda majina ya watu na kuleta maana.

## METHODOLOJIA

Data za makala haya ilikusanywa katika wilaya ya Mpwapwa na Chamwino mkoani Dodoma kwa kutumia mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa. Jumla ya watoataarifa arobaini na nane (48) waliteuliwa kimakusudi kutoka katika vijiji vya Mima, Gulwe, Mvumi Misheni, na Handali. Watoataarifa kumi na mbili (12) kutoka kila kijiji waliteuliwa kutokana na umahiri wa lugha ya Kiswahili na Kigogo pamoja na jinsia. Data za makala haya zimewasilishwa kwa kutumia majedwali na baadhi ya data zimewasilishwa kwa kutumia michorati ili kudadavua vyema mpangilio wa vipashio vinavyounda majina husika na kuonesha jinsi vipashio hivyo vilivyopangwa kidarajia kimsonge.

## UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Kipengele kilichojadiliwa katika uchunguzi wa mada ya makala haya ni uchambuzi wa maumbo na maana za majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo.

### Uchanganuzi wa Maumbo Yanayounda Majina ya Asili ya Watu katika Jamii-lugha ya Wagogo

Majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yanaweza kuainishwa katika maumbo ya aina mbili kisintaksia, yaani majina yenye muundo wa neno moja na majina ya watu yenye muundo wa maneno mawili au zaidi. Hata hivyo, lengo la makala haya ni kushughulikia majina ya watu yenye muundo wa neno moja pekee. Baada ya kuchunguza data tulionayo imebainika kwamba baadhi ya majina ya asili ya watu yenye muundo wa neno moja hujidhihirisha kama nomino.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Aidha, yapo majina kadhaa yanayojibainisha kama vitenzi licha ya kurejelea majina mbalimbali. Majina hayo ya asili ya watu yamejengwa kwa vipashio kadha wa kadha ambavyo kwa pamoja vinaungana ili kuunda jina moja la mtu. Sehemu zinazofuata zimeangazia maumbo mbalimbali yanayounda majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo.

**Maumbo ya Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo**

Kwa kuwa lengo la makala haya ni kuchambua maumbo na maana za majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo ni vyema kuangalia maumbo ya baadhi ya majina ya asili ya watu yanayotokana na makundi mbalimbali katika jamii husika. Makundi hayo ni kama yafuatavyo:

**Jedwali 1: Maumbo ya Majina ya Watu Yatokanayo na Matukio ya Vipindi au Misimu**

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| *-zeng-* | *Mazengo* | *Ma- zeng -o*<br>$K_{(a)}$ -Mz- $K_{(tno)}$ | Miti ya kujengea |
| | *Izengo* | *I - zeng- o*<br>$K_{(a)}$ -Mz-$K_{(tno)}$ | *Mti wa kujengea* |
| | *Nzengo* | *N- zeng- o*<br>$K_{(a)}$ - Mz- $K_{(tno)}$ | Jengo |
| | *Zengo* | *Ø - zeng- o*<br>$K_{(a)}$ - Mz- $K_{(tno)}$ | Jengo |
| | *Cizengo* | *Ci - zeng-o*<br>$K_{(a)}$ - Mz-$K_{(tno)}$ | Mti mdogo wa kujengea |
| *-belej-* | *Lubeleje* | *Lu -belej- e*<br>$K_{(a)}$ - Mz -$K_{(tno)}$ | Alizaliwa wakati wa kutoa mabua shambani |
| | *Mbeleje* | *M - belej-e*<br>$K_{(a)}$ -Mz -$K_{(tno)}$ | Alizaliwa wakati wa kutoa mabua shambani |
| | *Ibeleje* | *I - belej- e*<br>$K_{(a)}$ - Mz-$K_{(tno)}$ | Bua |
| | *Mabeleje* | *Ma -belej-e*<br>$K_{(a)}$ -Mz- $K_{(tno)}$ | Mabua |

Chanzo: Data ya Uwandani

Katika mchakato wa unominishaji, mzizi wa nomino umepokea viambishi awali husika na viambishi tamati ili kuunda nomino husika.

**Mfano 1:** Jina *Mazengo* lina maumbo (mofu) matatu ambayo ni umbo la kwanza ni “*Ma-*”, umbo la pili ni “*-zeng-*” na umbo la tatu ni “*-o*”.

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio vidogo hujenga vipashio vikubwa zaidi kupitia ngazi leksia.


**Kanuni:** $[K_{(a)}]+[Mz] + [K_{(tno)}] \rightarrow [N]n$

**Maelezo:** Kiambishi awali $[K_{(a)}]$ kinaunganishwa na mzizi wa nomino [Mz] pamoja na kiambishi tamati nominishi $[K_{(tno)}]$ na kuunda nomino mpya [N]n. Vipashio katika maumbo haya hupangwa kimsonge na kudhihirisha maumbo yafuatayo:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Kielelezo 1: Mpangilio wa Vipashio kimsonge Katika [$K_{(a)}$]+[Mz]+[$K_{(tno)}$]→[N]n**





**Mfano 2:** Jina "*Lubeleje"* ambalo lina maumbo (mofu) matatu ambayo ni umbo la kwanza ni *Lu*-, umbo la pili -*belej*- na umbo la tatu ambalo ni –e.

Jina la "*Lubeleje*" "*Ibelege*" hupewa mtoto wa kiume na wa kike hupewa jina la "*Mbeleje*" majina hayo hupewa mtoto ambaye amezaliwa kipindi au msimu wa kutayarisha mashamba kwa kuondoa mabua (*mabeleje*) kwa ajili ya kilimo cha msimu unaofuata.

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hizi hupangwa kimsonge ambapo vipashio vidogo hujenga vipashio vikubwa zaidi kupitia ngazi Leksia. Yaani kiambishi awali [$K_{(a)}$] huunganishwa na mzizi wa nomino [Mz] pamoja na kiambishi tamati kinominishi [$K_{(tno)}$] ili kuunda nomino mpya [N]n. Angalia kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo 2: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$] + [Mz]+ [$K_{(tno)}$ ] → [N]n**




Kulingana na *kielelezo 2* imebainika kuwa kiambishi awali [$K_{(a)}$] hufuata mzizi wa kitenzi [Mz] na kuungana na kiambishi tamati kinominishi [$K_{(tno)}$] na si kinyume ili kuunda nomino [N] husika.

**Jedwali 2: Maumbo ya Majina ya Watu Yatokanayo na Matukio ya Mungu**

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| *-lekwa* | *Kalekwa* | *Ka-lekwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | ameachwa |
| | *Mlekwa* | *M- lekwa*<br>$K_{(a)}$ -Mz | Ameachwa |
| | *Cilekwa* | *Ci- lekwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Tumeachwa |
| | *Ndekwa* | *Ø -ndekwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Nimeachwa |
| *-ciwa* | *Mciwa* | *M- ciwa*<br>$K_{(a)}$ -Mz | Mkiwa |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| | *Meciwa* | *Me- ciwa*<br>$K_{(a)}$- Mz | Mkiwa |
| | *Waciwa* | *Wa-ciwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Wakiwa |
| | *Uciwa* | *U -ciwa*<br>$K_{(a)}$- Mz | Ukiwa |
| *-solwa* | *Msolwa* | *M- solwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Amechukuliwa |
| | *Kasolwa* | *Ka- solwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Kachukuliwa |
| | *Cisolwa* | *Ci- solwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Tumechukuliwa |
| | *Wasolwa* | *Wa- solwa*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Wamechukuliwa |

Chanzo: Data ya Uwandani

Katika mchakato wa kuunda nomino mzizi wa wa kitenzi umepokea kiambishi awali ili kuunda nomino husika. Hebu tuchunguze mifano ifuatayo:

**Mfano 1:** Jina Kalekwa lina maumbo (mofu) mbili ambayo ni umbo la kwanza ni "*Ka-*" na umbo la pili ni "*-lekwa*" ambalo ndio mzizi wa kitenzi.


Jina "*Kalekwa*" linaonekana kutumika kwa jinsi zote mbili yaani kiume (me) na kike (ke). Jina hilo hutolewa kwa mtoto ambaye ni yatima aliyezaliwa wakati au baada ya kuzaliwa wazazi wake wote wawili walifariki dunia. Majina mengine ambayo hutolewa ni *Mlekwa*, *Cilekwa* na *Ndekwa*.

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksia vijenzi vya nomino hizi hupangwa kimsonge ambapo vipashio vidogo hujenga vipashio vikubwa zaidi kupitia ngazi Leksia.

**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz]→ [N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa kitenzi [Mz] na kuunda nomino [N] husika.

**Kielelezo 3: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$] + [Mz]→ [N]n**




Kulingana na *Kielelezo 3* imebainika kuwa kiambishi awali [$K_{(a)}$] hufuata mzizi wa kitenzi [Mz] na si kinyume ili kuunda nomino [N] husika.

**Mfano 2:** Jina *Msolwa* lina maumbo (mofu) mawili ambayo ni umbo "*M*" na umbo "*solwa*" ambalo ni mzizi wa kitenzi.

Jina "*Msolwa*" linaonesha kutumiwa kwa jinsi zote mbili yaani kiume (me) na kike (ke). Katika jamii-lugha ya Wagogo jina hilo hutolewa kwa mtoto ambaye wakati wa kuzaliwa au baada ya kuzaliwa


Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

kwake wazazi wake wote wawili walifariki au mzazi mmoja kati ya baba au mama. Pia wakati mwingine jina hili hutolewa kwa mtoto ili kurithi jina la mwanzilishi wa jina hilo ambaye ni ndugu wa karibu wa familia husika. Majina mengine ni *Kasolwa*, *Cisolwa* na *Wasolwa*.

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksia vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio hupitia katika ngazi Leksia.

**Maelezo**: Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa kitenzi [Mz] na kuunda nomino mpya [N]n. Angalia kielelezo kifuatacho ili kuona namna kanuni hii hutenda kazi.

**Kielelezo 4: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$]+ [Mz]→[N]n**




Mzizi “*solwa*” huambishwa kwa kiambishi awali “*m*” na kuunda nomino “*Msolwa*”

**Jedwali 3: Maumbo ya Majina ya Watu Yatokanayo na Mahali pa Kuzaliwa**

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| *-tunda* | *Itunda* | *I- tunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Mlima mkubwa |
| | *Matunda* | *Ma-tunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Milima |
| | *Citunda* | *Ci- tunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Mlima mdogo |
| | *Litunda* | *Li- tunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Mlima mkubwa |
| *-gunda* | *Mgunda* | *M- gunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Shamba |
| | *Cigunda* | *Ci- gunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Shamba dogo |
| | *Magunda* | *Ma- gunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Mashamba makubwa |
| | *Ligunda* | *Li- gunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Shamba kubwa |
| *-bago* | *Mbago* | *Ø- bago*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Pori |
| | *Ibago* | *I- bago*<br>$K_{(a)}$ -Mz | Pori kubwa |
| | *Cibago* | *Ci- bago*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Pori dogo |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| | *Mabago* | *Ma- bago*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Mapori |
| | *Libago* | *Li-bago*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Pori kubwa |

Chanzo: Data ya Uwandani

Kundi hili linahusisha kiambishi awali kinachounganishwa na nomino ili kuunda neno jipya aina ya nomino. Hebu tuchanganue maumbo ya nomino kwa kuangalia kazi na maana ya kila umbo kwa kuangalia mifano ifuatayo:


**Mfano 1:** Jina "*Citunda*" huundwa na maumbo (mofu) mawili ambayo ni umbo "*Ci-*" na umbo "*tunda*" ambalo ndio mzizi wa nomino.

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hizi hupangwa kimsonge kwa kupitia ngazi Leksia.

**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz]→[N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa nomino [Mz] na kuunda nomino [N] mpya. Angalia kielelezo kifuatacho kuona namna kanuni hii hutenda kazi:

**Kielelezo 5: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$] + [Mz]→[N]n**




Kulingana na *kielelezo 5* imebainika kuwa kiambishi awali [$K_{(a)}$] hufuata mzizi wa nomino [Mz] na kuunda nomino [N] husika.


**Mfano 2:** Jina "*Ibago*" lina maumbo (mofu) mawili ambayo ni umbo "*I*"na umbo "*bago*" ambalo huwakilisha mzizi wa nomino.

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio hujengwa kupitia ngazi Leksia kama ilivyo katika kanuni ifuatayo:

**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz] →[N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa neno [Mz] na kuunda nomino [N] mpya. Hebu tuchunguze kielelezo kifuatacho kuona namna kanuni hii hutenda kazi:

**Kielelezo 6: Mpangilio wa Vipashio Katika [$K_{(a)}$]+ [Mz]→[N]n**




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Kulingana *Kielelezo 6* imebainika kuwa kiambishi awali [$K_{(a)}$] hufuata mzizi wa nomino [Mz] na kuunda nomino [N] husika.

**Jedwali 4: Maumbo ya Majina ya Watu Yatokanayo na Matukio ya Majanga**

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| *-gay-* | *Magaya* | *Ma-gay-a*<br>$K_{(a)}$-Mz-$K_{(tno)}$ | Shida |
| | *Magayo* | *Ma- gay- o*<br>$K_{(a)}$- z- $K_{(tno)}$ | Shida |
| | *Lyagaya* | *Lya-gay-a*<br>$K_{(a)}$-Mz- $K_{(tno)}$ | Shida |
| | *Ngayo* | *N- gay- o*<br>$K_{(a)}$-Mz-$K_{(tno)}$ | Shida |
| | *Igayo* | *I- gay- o*<br>$K_{(a)}$-Mz- $K_{(tno)}$ | shida |
| -<br>gazw-<br>- | *Mgazwa* | *M- gaz-wa*<br>$K_{(a)}$- Mz-$K_{(tno)}$ | Sumbuliwa |
| | *Magazwo* | *Ma- gaz-wa*<br>$K_{(a)}$ -Mz- $K_{(tno)}$ | Msumbuko |
| | *Ngazwa* | *N- ga-zwa*<br>$K_{(a)}$-Mz-$K_{(tno)}$ | Sumbuliwa |
| *-suli-* | *Cisuligwe* | Ci- *suli*-gwe<br>$K_{(a)}$- Mz- $K_{(tno)}$ | Tumekataliwa |
| | *Suligwe* | *Ø- suli-gwe*<br>$K_{(a)}$ - Mz- $K_{(tno)}$ | Kataliwa |
| | *Msulice* | *M- suli-ce*<br>$K_{(a)}$-Mz- $K_{(tno)}$ | Mmekataliwa |
| tn | *Sulice* | *Ø- suli-* ce<br>$K_{(a)}$- Mz- $K_{(tno)}$ | Nimekataliwa |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Katika mchakato wa kuunda nomino mpya mzizi wa kitenzi umepokea kiambishi awali na kiambishi tamati ili kuunda nomino husika. Hebu tuchunguze mifano ifuatayo:

**Mfano 1:** Jina "*Lyagaya*" limeundwa na maumbo (mofu) matatu ambayo ni "*Lya-*", "*gay-*" na umbo "*a*".

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio hujengwa kwa kupitia ngazi Leksika kama ilivyo katika kanuni ifuatayo:


**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$]→[N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa kitenzi [Mz] pamoja na kiambishi tamati nominishi [$K_{(tno)}$] na kuunda nomino mpya [N]n.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Kielelezo 7: Mpangilio wa Vipashio Katika [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$]→[N]n**




Kulingana *Kielelezo 7* imebainika kuwa kiambishi awali [$K_{(a)}$] hufuata mzizi wa kitenzi [Mz] pamoja na kiambishi tamati nominishi [$K_{(tno)}$] na kuunda [N] husika.


**Mfano 2:** Jina "*Msulice*" huundwa na maumbo (mofu) matatu ambayo ni "*M-*", "*suli-*" na "*ce*".

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kwa kupitia ngazi Leksia kama ilivyo katika kanuni ifuatayo:

**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$]→ [N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na [Mz] wa kitenzi pamoja na kiambishi tamati kinominishi [$K_{(tno)}$] na kuunda nomino mpya [N]n.

**Kielelezo 8: Mpangilio wa Vipashio Katika [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$]→ [N]n**




Kulingana *Kielelezo 8* imebainika kuwa kiambishi awali, hufuata mzizi wa kitenzi pamoja na kiambishi tamati nominishi na kuunda nomino husika.

**Jedwali 5: Maumbo ya Majina ya Watu Yatokanayo na Matendo ya Watu**

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| *-sek-* | *Seko* | *Ø- sek- o*<br>$K_{(a)}$- Mz- $K_{(tno)}$ | Cheko |
| | *Maseko* | Ma- sek- o<br>$K_{(a)}$ -Mz- $K_{(tno)}$ | Cheko |
| | *Msekwa* | *M- sek- wa*<br>$K_{(a)}$- Mz- $K_{(tno)}$ | Anayechekwa |
| | *Mseci* | *M- sec- i*<br>$K_{(a)}$ - Mz- $K_{(tno)}$ | Mcheshi |
| -<br>*nene-* | *Cinenelwa* | *Ci-nene-lwa*<br>$K_{(a)}$-Mz- $K_{(tno)}$ | Tumesamehewa |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| | *Cinenei* | *Ci-nene- i*<br>$K_{(a)}$ -Mz-$K_{(tno)}$ | Kisamehewa |
| | *Nenelwa* | *Ø-nene-lwa*<br>$K_{(a)}$-Mz-$K_{(tno)}$ | nimesamehewa |
| | *Mnenelwa* | *M-nene-lwa*<br>$K_{(a)}$-Mz- $K_{(tno)}$ | Msamehewa |
| *-jend-* | *Majenda* | *Ma-jend-a*<br>$K_{(a)}$- Mz- $K_{(tno)}$ | Mtembezi |
| | *Mijendi* | *Mi-jend- i*<br>$K_{(a)}$-Mz- $K_{(tno)}$ | Matembezi |
| | *Mjendi* | *M-jend-i*<br>$K_{(a)}$-Mz-$K_{(tno)}$ | Mtembezi |
| | *Cijendi* | Ci-*jend-i*<br>$K_{(a)}$-Mz-$K_{(tno)}$ | Kitembezi |

Chanzo: Data ya Uwandani

Katika mchakato wa kuunda nomino kiambishi awali kinaungana na mzizi wa kitenzi pamoja na kiambishi tamati kinominishi na kuunda nomino husika. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:


**Mfano**1**:** Jina "*Maseco*" huundwa na maumbo matatu ambayo ni umbo "*ma*", "*sek*" na "*o*".

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio hujengwa kupitia ngazi Leksia. Hebu tuangalie kanuni ifuatayo ili tuone namna ambavyo hutenda kazi:

**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$]→ [N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa kitenzi [Mz] pamoja na kiambishi tamati nominishi [$K_{(tno)}$] na kuunda nomino [N] husika.

**Kielelezo 9: Mpangilio wa Vipashio Katika [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$K]→[N]**




Kutokana na *Kielelezo 9* imebainika kuwa kiambishi hufuata mzizi wa kitenzi pamoja na kiambishi tamati kinomishi na kuunda nomino husika.

**Mfano 2:** Jina "*Cinenelwa*" limeundwa na maumbo (mofu) matatu ambayo ni "*ci-*", "*nene-*" na "*lwa*".

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio hujengwa kwa kupitia ngazi Leksia kama ilivyo katika kanuni ifuatayo:


**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$] → [N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaungana na mzizi wa kitenzi [Mz] pamoja na kiambishi tamati kinominishi [$K_{(tno)}$] na kuunda nomino [N] mpya.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Kielelezo 10: Mpangilio wa Vipashio Katika [$K_{(a)}$] + [Mz] + [$K_{(tno)}$] → [N]**




Kutokana na *Kielelezo 10* imebainika kuwa kiambishi awali hufuata mzizi wa kitenzi pamoja na kiambishi tamati nominishi na kuunda nomino husika.

**Jedwali 6: Majina ya Watu Yatokanayo na Majina ya Ndege**

| Mzizi | Nomino | Maumbo | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| *-nghwezi* | *Nyanghwezi* | *Nya-nghwezi*<br>$K_{(a)}$- Mz | Ndege tausi |
| | *Manghwezi* | Ma-nghwezi<br>$K_{(a)}$- Mz | Wingi wa ndege tausi |
| | *Nghwezi* | *Ø-nghwezi*<br>$K_{(a)}$- Mz | Tausi |
| -nhwale | *Nhwale* | *Ø-nhwale*<br>$K_{(a)}$- Mz | Kwale |
| | *Cinhwale* | *Ci-nhwale*<br>$K_{(a)}$- Mz | Kwale mdogo |
| | *Manhwale* | *Ma-nhwale*<br>$K_{(a)}$- Mz | Kwale wengi |
| -ndeje | *Mandege* | *Ma-ndeje*<br>$K_{(a)}$- Mz | Ndege wengi |
| | *Cindeje* | *Ci-ndeje*<br>$K_{(a)}$- Mz | Ndege mdogo |
| | *Nyandeje* | Nya-ndeje<br>$K_{(a)}$ - Mz | Ndege |
| | *Ndeje* | ***Ø-ndeje***<br>**Maumbo** | **Ndege**<br>**Maana kwa Kiswahili** |
| | | $K_{(a)}$- Mz | |

Chanzo: Data ya Uwandani

Katika mchakato wa kuunda nomino mzizi wa nomino umepokea kiambishi awali na kuunda nomino mpya. Hebu tuchunguze mifano ifuatayo:

**Mfano 1:** Jina "*Nyanghwezi*"ni jina ambalo limeundwa na maumbo (mofu) mawili ambayo ni "*nya-*" na "*nghwezi*".

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio hujengwa kwa kupitia ngazi Leksia kama ilivyo katika kanuni ifuatayo:


**Kanuni: [$K_{(a)}$] + [Mz] → [N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaungana na mzizi [Mz] wa nomino [N] na kuunda nomino mpya.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Kielelezo 11: Mpangilio wa Vipashio Katika [$K_{(a)}$] + [Mz]→[N]n**




Kutokana na *Kielelezo 11* imebainika kuwa kiambishi awali hufuata mzizi wa nomino na kuunda nomino mpya.


**Mfano 2:** Jina *Mandeje* limeundwa na maumbo (mofu) mawili ambayo ni "*ma-*" na "*ndeje*".

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksika vijenzi vya nomino hupangwa kimsonge ambapo vipashio hujengwa kwa kupitia ngazi Leksia kama ilivyo katika kanuni ifuatayo:

**Kanuni: [$K_{(a)}$] +[Mz]→ [N]n**

**Maelezo:** Kimbishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa nomino [Mz] na kuunda nomino [N] mpya.

**Kielelezo 12: Mpangilio wa Vipashio katika [$K_{(a)}$] + [Mz]→ [N**




Kulingana na *Kielelezo 12* imebainika kuwa kiambishi awali hufuata mzizi wa nomino ili kuunda nomino mpya.

**Majina ya Watu ya Jamiilugha ya Wagogo Yanayojidhirisha Katika Umbo la Nomino**

Majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yenye muundo wa nomino yanajidhihirisha katika maumbo ya aina mbili. Maumbo ya majina yasiyonyambuliwa na majina yenye kubeba viambishi-nyambulishi na majina yale yenye kuonesha mwambatano. Majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yanayotokana na nomino kwa asili yake hujibainisha katika maumbo mbalimbali. Maumbo yaliyobainishwa ni kama yafuatavyo:

***Maumbo ya Kiambishi – Awali na Mzizi***

Majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo katika aina hii ya uundaji wa majina huunganishwa na kiambishi awali na mzizi ili kuunda jina moja linalowakilisha dhana moja.

**Kanuni: [$K_{(a)}$] +[ $M_z$]→ [N]$_n$**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na mzizi wa neno [Mz] na kuunda nomino [n]$_n$. Kama mifano katika *Jedwali 7* linavyoonesha:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227


**Jedwali 7: Mifano ya Majina ya Watu Yenye Maumbo ya [$K_{(a)}$]+ [Mz]**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Mlekwa* | *M – lekwa*<br>$K_{(a)}$- Mz | Kuachwa |
| *Matunda* | *Ma – tunda*<br>$K_{(a)}$ - Mz | Milima |
| *Ihanze* | *I – hanze*<br>$K_{(a)}$-Mz | jani |
| *Mabici* | Ma – bici<br>$K_{(a)}$ - Mz | Miti mikubwa |
| *Udoba* | U– *doba*<br>$K_{(a)}$-Mz | Uvivu |
| *Cibehe* | *Ci – behe*<br>$K_{(a)}$- Mz | Kivuli |
| *Cipegwa* | Ci – pegwa<br>$K_{(a)}$ -Mz | Tumepewa |

**Chanzo**: Data za Uwandani

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksia vijenzi vya nomino hizi hupangwa kimsonge ambapo vipashio vidogo hujenga vipashio vikubwa zaidi kupitia ngazi Leksia. Angalia kielelezo kifuatacho uone namna kanuni hii hutenda kazi:

**Kielelezo 13: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$+Mz]**




Kama *Kielelezo 13* kinavyoonesha majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yenye maumbo ya kiambishi awali na mzizi yameundwa na vipashio vilivyopangwa kimsonge kama Nadharia ya Mofolojia Leksia inavyoeleza.

***Maumbo ya Kiambishi Awali cha Ukubwa na Mzizi***

Baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yameundwa na viambishi awali vya ukubwa ambavyo hujitokeza katika baadhi ya nomino ambazo huonesha ukubwa katika lugha ya Kigogo. Majina hayo yameundwa na kiambishi awali cha ukubwa [$K_{(a/u)}$] na mzizi wa nomino [Mz]. Kanuni inayotumika ni:

**Kanuni: [$K_{(a/u)}$] + [Mz]→[N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali cha ukubwa [$K_{(a/u)}$] kinaungana na mzizi wa nomino [Mz] na kuunda [N]n kama *Jedwali 8* linavyoonesha:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227


**Jedwali 8: Mifano ya Majina ya Watu Yenye Maumbo ya [$K_{(a/u)}$] + [Mz]**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Igundu* | *I – gundu*<br>$K_{(a/u)}$ - Mz | Bustani kubwa |
| *Malamba* | *Ma – lamba*<br>$K_{(a/u)}$ - Mz | Mito mikubwa |
| *Ligunda* | *Li – gunda*<br>$K_{(a/u)}$ - Mz | Shamba kubwa |
| *Ibago* | *I – bago*<br>$K_{(a/u)}$- Mz | Pori kubwa |
| *Matunda* | *Ma – tunda*<br>$K_{(a/u)}$- Mz | Milima mikubwa |
| *Isanzu* | *I – sanzu*<br>$K_{(a/u)}$ -Mz | Tawi kubwa |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Kama mifano inavyoonekana katika *Jedwali 8* majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo katika kategoria hii yameundwa na viambishi tangulizi *"i-"*,"li-"na "ma-"ambavyo vinavyojitokeza. Inaonesha kuwa majina ya watu ya jamii-lugha ya Wagogo yenye maumbo ya kuonesha ukubwa yameundwa na viambishi awali vinavyooonesha ukubwa na mzizi wa nomino husika. Aidha majina ya watu katika kategoria hii yameundwa na vipashio vidogo ambavyo kwa pamoja vimeunda majina ya watu kupitia ngazi leksia. Angalia kielelezo kifuatacho uone namna kanuni hii hutenda kazi.

**Kielelezo 14: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika Kiambishi [$K_{(a/u)}$] + [Mz]**




*Kielelezo 14* kinaonesha majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yenye maumbo ya kiambishi awali cha ukubwa na mzizi wa nomino yameundwa na vipashio vilivyopangwa kimsonge kama inavyodhihirishwa na Nadharia ya Mofolojia Leksika.

**Maumbo ya Kiambishi Awali cha Udogo na Mzizi wa Nomino**

Baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yanayoonesha maumbo ya kiambishi awali cha udogo ambayo hujitokeza na kuoneshwa kwa kutumia viambishi awali "ci-" na "vi-" vyenye kuashiria udogo. Majina hayo yameundwa na kiambishi awali cha udogo [$K_{(a/d)}$] na mzizi wa nomino [Mz]. Kanuni inayohusika ni:

**Kanuni: [$K_{(a/d)}$] + [Mz]→[N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali cha udogo [$K_{(a/d)}$] kinaungana na mzizi wa nomino [Mz] na kuunda [N]n kama inavyooneshwa katika *Jedwali 9*.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227


**Jedwali 9: Mifano ya Majina ya Watu Yenye Maumbo [K(a/d)] + [Mz]**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Cibada* | *Ci – bada*<br>$K_{(a/d)}$- Mz | Kibuyu kilichopasuka |
| *Vitunda* | *Vi – tunda*<br>$K_{(a/d)}$- Mz | Vilima vidogo |
| *Cisanzu* | *Ci – sanzu*<br>$K_{(a/d)}$ - Mz | Tawi dogo |
| *Vigundu* | *Vi – gundu*<br>$K_{(a/d)}$ - Mz | Vibustani vidogo |
| *Cigunda* | *Ci – gunda*<br>$K_{(a/d)}$- Mz | Shamba dogo |
| *Cibago* | *Ci – bago*<br>$K_{(a/d)}$- Mz | Pori dogo |
| *Vihali* | *Vi – hali*<br>$K_{(a/d)}$ - Mz | Sahani ndogo za kibuyu |

Chanzo: Data ya Uwandani

Mifano katika *Jedwali 9* inaonesha kuwa majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yenye maumbo ya kiambishi awali cha udogo na mzizi yameundwa na kiambishi awali "*ci*-" na "vi-". Kwa mujibu wa taarifa zilizokusanywa uwandani, majina hayo yalitokana na vitu vyenye sifa ya udogo, umoja na wingi wa vitu ambavyo vilikuwepo katika jamii husika. Tuchunguze kielelezo kifuatacho kuona namna kanuni inavyotumika:

**Kielelezo 15: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a/d)}$] + [Mz]**




Uundaji wa majina hayo kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika hujitokeza pale ambapo kiambishi awali kinachonesha udogo kinapoungana na mzizi wa nomino husika huunda nomino mpya kama kanuni ilivyotumika.

## Majina Nyambulishi

Baadhi ya majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yaliyokusanywa yametokana na vitenzi. Tofauti na majina mengine yaliyoshughulikiwa awali, majina ya watu katika kategoria hii yameundwa kutokana na unyambulishaji wa vitenzi. Majina ya watu yanayotokana na vitenzi yanajidhihirisha katika maumbo tofauti tofauti ambayo ni maumbo yanaundwa na kiambishi awali, mzizi na kiambishi tamati nominishi. Mifano ya maumbo hayo imefafanuliwa katika sehemu inayofuata.

### *Maumbo ya Kiambishi Awali, Mzizi na Kiambishi Tamati Nominishi*

Katika data tuliyonayo imebainika kuwa kuna baadhi ya majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yanayotokana na mashina au mizizi ya vitenzi hujidhihirisha katika maumbo ya kiambishi awali au mizizi ya vitenzi na kiambishi nominishi. Kanuni

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

inayoonesha

**Kanuni: [$K_{(a)}$ + Mz + $K_{(tno)}$] → [N]n**

**Maelezo**: Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaungana na mzizi wa kitenzi [Mz] pamoja na kiambishi tamati kinominishi [$K_{tno}$] na kuunda [N]n kama inavyoonesha katika *Jedwali 10*.

**Jedwali** 10**: Maumbo ya Kiambishi awali, Mzizi na Kiambishi Nominishi [$K_{(a)}$ + Mz +$K_{(tno)}$]**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Ilimo* | *I - lim - o*<br>$K_{(a)}$- Mz- $K_{(tno)}$ | Kulima |
| *Cizengo* | *Ci - zeng - o*<br>$K_{(a)}$ - Mz - $K_{(tno)}$ | Mti mdogo wa kujengea |
| *Ilumbo* | *I – lumb - o*<br>$K_{(a)}$- Mz - $K_{(tno)}$ | Shukurani |
| *Mazengo* | *Ma – zeng -o*<br>$K_{(a)}$ - Mz - $K_{(tno)}$ | Miti ya kujengea |
| *Izengo* | *I - zeng - o*<br>$K_{(a)}$ - Mz - $K_{(tno)}$ | Jengo |
| *Mkung'ano* | *M - kung'an - o*<br>$K_{(a)}$ - Mz - $K_{(tno)}$ | Mkutano |
| *Maseko* | *Ma – sek - o*<br>$K_{(a)}$ - Mz - $K_{(tno)}$ | Kicheko |
| *Mgunda* | *M – gund - a*<br>$K_{(a)}$ - Mz - $K_{(tno)}$ | Shamba |
| Isajilo | *I – sajil – o*<br>$K_{(a)}$ - Mz - $K_{(tno)}$ | Mashine |


Chanzo: Data ya Uwandani

Baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo kama yanavyoonekana katika *Jedwali 10* majina hayo yameundwa kutokana na unyambulishi wa vitenzi ambapo viambishi-awali, mzizi wa kitenzi na viambishi tamati nominishi vimeshirikiana ili kuunda majina husika. Viambishi nominishi vinavyojenga majina hayo ni kiambishi nominishi -o na kiambishi nominishi -a ambavyo vimepachikwa baada ya mzizi wakati viambishi awali vimepachikwa kabla ya mzizi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, viambishi hivi vimewekwa katika kundi la viambishi vyenye athari, yaani viambishi ambavyo husababisha badiliko la kiumbo hivyo kusababisha badiliko la kidhana. Aidha majina ya watu katika kategoria hii yameundwa na vipashio vidogo vidogo ambavyo kwa pamoja vimeunda majina ya watu kupitia katika mchakato wa unyambulishaji unaozingatia kanuni dhahiri ambao hutokea katika ngazi Leksia ya pili. Vipashio vinavyounda majina yenye maumbo ya kiambishi awali, mzizi na kiambishi tamati nominishi vimepangwa katika ngazi Leksia na kudhihirisha maumbo yafuatao:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Kielelezo 16: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$+Mz+ $K_{(tno)}$]**




Majina ya watu katika kategoria hii yametokana na mashina ya vitenzi. Hivyo basi, shina la kitenzi huundwa kwanza na kisha kupitishwa katika ngazi ya pili ambapo viambishi awali na viambishi nominishi hupachikwa katika shina husika. Upachikaji wa viambishi hivyo hutokana na mchakato wa unyambulishaji dhahiri ambao kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika hufanyika katika ngazi ya pili. Kwa hiyo, viambishi awali na viambishi tamati nominishi hushirikiana katika kuunda majina ya watu yanayotokana na unominishaji. Kama *Kielelezo 16* kinavyoonesha vipashio vinavyojenga maumbo mbalimbali ya majina ya watu vimepangwa kimsonge kama hatua kwa hatua ili kukamilisha azma za kuunda jina husika.

## Majina ya Watu Yenye Maumbo ya Vitenzi

Kulingana na uchanganuzi wa data tuliyonayo imebainika kuwa kuna baadhi ya majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo kama yalivyo majina ya watu ya Kiswahili, yana maumbo ya vitenzi. Majina haya yamedhihirisha ruwaza mbalimbali za vitenzi licha ya kurejelea majina ya watu fulani. Ruwaza hizo ni viambishi awali vya nafsi, mzizi wa kitenzi, viambishi tamati vya unominishaji na kadhalika. Hebu tuangalie maumbo yafuatayo:

### *Maumbo ya Kiambishi Awali cha Nafsi, Mzizi na Irabu Ishilizi*

Katika aina hii ya uundaji wa nomino huundwa kwa kuunganisha kiambishi cha nafsi, mzizi wa kitenzi na irabu ishilizi. Maumbo haya huundwa kwa kanuni ifuatayo:

**Kanuni: [$K_{(a/n)}$ +Mz + I ] → [N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali cha nafsi [$K_{(a/n)}$] inaungana na [Mz] pamoja na [I] irabu ishilizi na kuunda [N]n nomino mpya. Tuchunguze mifano ya majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yanavyoundwa kwa utaratibu huu kama *Jedwali 11* linavyoonesha:

**Jedwali 11: Maumbo ya Kiambishi Awali cha Nafsi, Mzizi na Irabu [K(a/n)+Mz + I]**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Kuhodanga* | *Ku-hodang-a*<br>$K_{(a/n)}$ - Mz- I | Umeharibu |
| *Mapujila* | *Ma - pujil- a*<br>$K_{(a/n)}$ - Mz- I | Mdhulumashi |
| *Magawa* | *Ma - gaw- a* | Mgawaji |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.


Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

| | | |
|---|---|---|
| | $K_{(a/n)}$ - Mz- I | |
| *Mpelembi* | *M - pelemb- i*<br>$K_{(a/n)}$ - Mz- I | Mwindaji |
| *Cilongani* | *Ci-longan- i*<br>$K_{(a-n)}$ -Mz- I | Tusemezane |
| *Mwanika* | *Mwa-nik- a*<br>$K_{(a/n)}$ - Mz- I | Mwanikaji |
| *Suligwe* | *Su- ligw- e*<br>$K_{(a/n)}$ - Mz- I | Chukiwa |
| *Makanyaga* | *Ma-kanyag-a*<br>$K_{(a/n)}$ - Mz-I | Mkanyagaji |
| *Mgonela* | *M-gonel- a*<br>$K_{(a/n)}$- Mz- I | Mlalia |
| *Mnyanyi* | *M- nyany- i*<br>$K_{(a/n)}$- Mz- I | Mchomeleaji |

Chanzo: Data ya Uwandani

Mifano katika *Jedwali 11* imebainika kuwa baadhi ya majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo huwa na maumbo ya kiambishi awali cha nafsi [$K_{(a/n)}$], mzizi wa kitenzi [Mz] na irabu ishilizi [I] vikiunganishwa huunda nomino mpya. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, vipashio vinavyounda maneno vimepangwa kidarajia kimsonge, kipashio kimoja na kingine ili kuunda kipashio kikubwa zaidi na kudhihirishwa na maumbo yafuatayo:

**Kielelezo 17: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a/n)}$ + Mz +I]**




Kielelezo hiki kinaonesha kinaonesha kuwa licha ya majina ya kundi hili kuwa vitenzi, maumbo yake yamezingatia upangaji wa vipashio kwa ngazi leksika. Hivyo basi, vipashio vidogo ambavyo ni mzizi ***-hodang-*** na irabu ishilizi ***-a*** vimeungana na kuunda shina la kitenzi '*hodanga'* na kiambishi nafsi ***ku*** kimeunganika na shina la kitenzi '*hodanga'* na kuunda kitenzi *Kuhodanga* ambacho kimetumika kama jina la mtu.

***Maumbo ya Kiambishi awali, Mzizi wa Kitenzi, Kiambishi cha Utendwa na Irabu ishilizi [$K_{(a)}$+Mz+tdw+I]***

Katika utafiti huu imebainika kuwa kuna baadhi ya majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yenye maumbo ya kiambishi awali, mzizi au shina, kiambishi cha utendwa na irabu ishilizi. Kanuni ya

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

muundo huu ni:

**Kanuni: [$K_{(a)}$ + Mz+ tdw + I ]→ [N]n**

**Maelezo:** Kiambishi awali ($K_{(a)}$), mzizi (Mz), kiambishi cha utendwa (tdw) na vikiunganishwa na irabu ishilizi (I) kuunda nomino mpya. Mifano ya vitenzi vilivyoundwa kwa utaratibu huo ni vinaoneshwa na *Jedwali 12* kama ifuatavyo:


**Jedwali 12: Majina ya Watu Yenye Maumbo Katika [K(a) + Mz +tdw +I]**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Mwendwa* | *Mw-end-w- a*<br>$K_{(a)}$ -Mz -tdw-I | Pendwa |
| *Mlekwa* | *M- lek- w- a*<br>$K_{(a)}$-Mz-tdw-I | Achwa |
| *Kalekwa* | *Ka-lek- w - a*<br>$K_{(a)}$-Mz-tdw-I | Kaachwa |
| *Hadikwa* | *Ha-dik-w - a*<br>$K_{(a)}$-Mz-tdw-I | Pandwa |
| *Mgazwa* | *M-gaz-w- a*<br>$K_{(a)}$- Mz-tdw-I | Sumbuliwa |
| *Mkumbukwa* | *M-kumbuk-w-a*<br>$K_{(a)}$-Mz-tdw-I | Kumbukizi |
| *Cadigwa* | *Ca-dig- w- a*<br>$K_{(a)}$-Mz-tdw-I | Chakula |
| *Msekwa* | *M-sek-w- a*<br>$K_{(a)}$-Mz-tdw-I | kumbukwa |
| *Cipegwa* | *Ci -peg- w- a*<br>$K_{(a)}$-Mz-tdw-I | tumepewa |
| *Mbezwa* | *Mu-bez-w- a*<br>$K_{(a)}$- Mz- tdw-I | Kataliwa |

Chanzo: Data ya Uwandani

Mifano katika *Jedwali 12* inadhihirisha kuwa majina katika kategoria hii yameundwa na kubainishwa katika maumbo ya kiambishi awali, mzizi, kiambishi cha utendwa na irabu ishilizi ili kuunda nomino moja. Uundaji wa majina haya pia umeongozwa na mhimili wa Nadharia ya Mofolojia Leksika unaozingatia kuundwa kwa vipashio vidogovidogo ambavyo vimepangwa katika ngazi Leksia kimsonge.

**Kielelezo 18: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$ +Mz +tdw + I]**




 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Kielelezo hiki kinafafanua kuwa vipashio vidogo kama vile kiambishi awali ***M-*** na mzizi ***sek-*** vimeshirikiana na kiambishi cha utendewa ***w-*** na irabu ishilizi ***-I*** na kuunda kitenzi '*Mulekwa'* ambacho kinatumika kama nomino mpya.

**Nomino Ambatani Sahili**

Nomino ambatani sahili ni maumbo ya majina yaliyoundwa kwa vijenzi viwili tu. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mofolojia Leksika, vijenzi hivi huwa tayari vimeundwa katika mzunguko wa kwanza au wa pili kabla ya kupitishwa katika ngazi ya pili ambapo huambatishwa kwa kutumia lugha inayohusika (Kiparsky, 1982; Mcmahon, 2000).

Kulingana na uchanganuzi wa data tumebaini kuna makundi yenye maumbo sahili tukizingatia kigezo kulingana cha aina ya maneno yanayohusika na namna yalivyopangwa katika umbo. Maumbo hayo ni:

***Maumbo ya Nomino na Nomino***

Katika aina hii ya uundaji wa majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo, nomino mbili zinaungana na kuunda neno moja aina ya nomino linalowakilisha dhana moja. Kanuni ya mwambatano inayohusika ni:

**Kanuni:** $[K_1]_N + [K_2]_N \rightarrow [[K]_N[K]_N]_N$

**Maelezo:** Nomino $[K_1]$ inaunganishwa na nomino $[K_2]$ na kuunda nomino moja.

Mhimili wa kufuta mabano umetumiwa kuonesha bayana utaratibu wa kujenga neno kamili kwa kutumia vijenzi vyake. Zingatia mifano ifuatayo kutoka kwa data yetu:


**Jedwali 13: Mifano ya Majina ya Watu Yenye Maumbo ya [K1]N + [K2]N**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Ndejeulaya* | *Ndeje – ulaya*<br>$K_1$ $K_2$ | Ndege ya abiria |
| *Munyawusi* | *Munya-wusi*<br>$K_1$ $K_2$ | mwananchi |
| *Musilikale* | *Musili-kale*<br>$K_1$ $K_2$ | mwanajeshi |
| *Lomolomo* | *Lomo - lomo*<br>$K_1$ $K_2$ | mdomo |

Chanzo: Data ya Uwandani

Kulingana na Nadharia ya Mofolojia Leksia vijenzi vya nomino hizi hupangwa kimsonge ambapo vipashio vidogo hujenga vipashio vidogo hujenga vipashio vikubwa zaidi kupitia ngazi Lekisia. Angalia kielelezo kifuatacho uone namna kanuni hii hutenda kazi.

**Kielelezo 19: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika $[NN]_N$**



Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Uundaji wa nomino ambatani kwa mujibu wa Mofolojia Leksika hutumia maneno kamili kama vijenzi (Libben, 2006). Kwa hiyo mwambatano hutokea wakati wa kuunganisha nomino (*ndeje* + *ulaya*). Hata hivyo vijenzi hivyo huwa tayari vimeundwa kimsonge kwa vijenzi vidogo zaidi yaani mofimu (*nde*+*je*) kwa kijenzi *Ndeje* na (*ulaya*) kwa kijenzi *ulaya*. Maneno '*ndeje'* na '*ulaya'* hupitishwa katika ngazi ya pili na kuambatishwa kwa kutumia kanuni ya lugha. Katika nomino ambatani zilizoundwa mofmu ambazo hazijaambishwa.

**Nomino Zinazoundwa na Majina Yenye Uradidi**

Majina yenye uradidi ni nomino ambazo zinaundwa kutokana na kurudiwa rudiwa ama kwa silabi au neno. Katika makala haya imebainika kuwa kuna majina ya watu yenye maumbo ya uradidi katika jamii-lugha ya Wagogo lakini majina hayo ni machache ambayo hutumika kwa jamii hiyo.

***Maumbo ya Majina ya Watu Yenye Uradidi wa Neno [$K_{(a)}$+$Mz_1$ +$Mz_2$]***

Baadhi ya majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yenye uradidi wa neno yameundwa na kiambishi awali na kufuatiwa na mizizi miwili inayofanana ili kupata nomino mpya. Maneno yanaundwa kwa utaratibu ufuatao:

**Kanuni: [$K_{(a)}$ + $Mz_1$ +$Mz_2$] → $[N]_N$**

**Maelezo:** Kiambishi awali [$K_{(a)}$] kinaunganishwa na neno la kwanza [$Mz_1$] na neno la pili [$Mz_2$] ili kuunda nomino mpya. Angalia mifano kutokana na *Jedwali 14* kama ifuatavyo:

**Jedwali 14: Mifano ya Majina ya Watu Yenye Uradidi wa Neno [K(a) + Mz1 +Mz2]**

| Nomino za Kigogo | Vijenzi vyake | Maana kwa Kiswahili |
|---|---|---|
| *Ilomolomo* | *I* – *lomo*- lomo<br>$K_{(a)}$ - $Mz_1$- $Mz_2$ | domo domo |
| *Imulimuli* | *I* – *muli*- *muli*<br>$K_{(a)}$- $Mz_1$- $Mz_2$ | radi |
| *Mlomolomo* | *M – lomo-lomo*<br>$K_{(a)}$ - $Mz_1$- $Mz_2$ | Mdomo mdomo |
| *Cing'aling'ali* | *Ci*- *ng'ali*-*ng'ali*<br>$K_{(a)}$ - $Mz_1$- $Mz_2$ | King'aling'ali |


Chanzo: Data za Uwandani

Mifano katika *Jedwali 14* inaonesha kuwa baadhi ya majina ya watu yenye uradidi wa neno yameundwa kwa maumbo ya kiambishi awali tofauti tofauti na mizizi miwili. Viambishi vinavyounda majina hayo ni ***"I"*** kama inavyoonekana katika mfano wa (1 na 2), "***m-***" katika mfano wa 3 na "***ci-"*** katika mfano 4. Majina ya watu yenye maumbo hayo katika jamii-lugha ni machache. Kwa hiyo, vipashio vinavyounda majina yenye maumbo ya kiambishi awali na mizizi miwili vimepangwa kimsonge na kudhihirisha maumbo yafuatayo:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Kielelezo 20: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika [$K_{(a)}$+$Mz_1$+ $Mz_2$]**




Kielelezo hiki kinadhihirisha kuwa majina ya watu katika kategoria hii yameundwa na vipashio vilivyopangwa kimsonge ambapo vipashio vidogo vimeungana na kuunda kipashio kikubwa zaidi. Uundaji wa majina haya pia umeongozwa na mhimili wa Nadharia ya Mofolojia Leksika unaozingatia kuwa leksimu huundwa na vipashio vidogo vidogo ambavyo vimepangwa katika ngazi Leksia kimsonge.

## HITIMISHO

Makala haya yamewakilisha uchanganuzi wa vijenzi vinavyounda majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo na kanuni zinazotawala vijenzi hivyo zimefafanuliwa. Uchanganuzi wa data katika makala haya umeongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksika hususani mhimili wa ngazi Leksika. Uchanganuzi umebaini kuwa majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yanayojibainisha katika maumbo ya neno moja moja yameundwa na vijenzi mbalimbali vilivyopangwa kidarajia kimsonge.

## MAREJELEO

Abdul, A. (2013). *Maana na Sababu za Kiisimujamii Kwenye Majina ya Koo za Kiluguru*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Agard, F.B. (1984). *A Course in Romance Linguistics: A Synchronic View.* USA: Georgetown University Press.

Allen, G. V. (1978). *Using the Written Language Creatively*. The Ohio State University, Marion.

Anusa, C. A. (2016). *Maana za Majina ya Watu Katika Jamii ya Wayao*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Aronoff, M. & Fudeman, K. (2011.) *What is morphology?* (2nd ed.). USA: Wiley- Blackwell.

Azael, R. (2013). *Maana za Majina ya Asili Katika Jamii ya Kiuru* (Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam).

Baitan, B. (2010). *Morphosemantic Analysis of Ruhaya Person Names* (M.A Dessertation University of Dar-es-salaam, Tanzania).

Buberwa, A. (2017). *Ruwaza za Kimofolojia za Majina ya Mahali ya Kihaya: Mtazamo wa Mofolojia Leksika*. Tasnifu ya shahada ya Uzamivu. Dar -es-Salaam, Chuo Kikuu cha Dar -es- Salaam.

Davis, E. M. (2016). *Majina ya Asili ya Vitongoji Yanayoitambulisha Jamii ya Wajita*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Gichuru, T.M. (2010). *Uchunguzi wa Nomino ambatani za Kiswahili*: *Mtazamo wa Mofolojia Leksia*. Tasnifu ya shahada ya uzamili Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, ir -library.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Kiparsky, P. (1982). *Lexical phonology and Morphology*. Encyclopedia of Language and Linguistics, 94-97. https//doi.org/10.1016/bo-08-044854-2/0008.

Manyasa, J. (2010). *Investigating the Basis of Naming People in Kisukuma*. M.A. Dessertation, University of Dar-es-Salaam, Tanzania.

Mascaro, J. (1979). *Catalan Phonology and Phonological Cycle*. *PhD Dissertation, M.I.T.* Reproduced by the Indiana University Linguistics Club.

Mcmahon, A. (2000). *Lexical Phonology and History of English. Cambridge*: Cambridge University Press.

Msanjila & Wenzake, (2009). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo.* TUKI. Dar es Salaam.

Nyangawa, M. (2013). *Uchunguzi wa Kisemantiki na Taratibu za Utoaji wa Mjina ya Kijita.* Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Pesetsky, D. (1976). "*Russian Morphology and Lexical Theory*". Ms. M.I.T.

Resani, M. (2014). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*, Dar. Karljamer Print Technology.

Rubach, J. (1981). *Syclic and Lexical Phonology*: *The Structure of Polish*. USA: Foris Publications.

Rugemalira, J.M (2005). *A Grammar of Runyambo*, Dar -es- Salaam: Language of Tanzania Project, University of Dar es Salaam.

Salapion, D. (2011). *Haja ya Kuunda Kamusi ya Majina ya Watu ya Asili: Majina ya Asili katika Jamii ya Wahaya*. Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Siegel, D. (1974). *Topics in English Morphology*, PhD. Dissertation, M.I.T. Siegel, D. (1977). "The Adjacency Condition and the Theory o f Morphology". In Proceedings of the Eighth Annual Meeting of the North East Linguistic Society, Amherst, Mass.

Tegisi, N. M (2019). *Uchunguzi wa Kisemantiki wa Majina ya Asili Katika Koo za Ginantuzu*. Tasnifu ya shahada ya Uzamivu. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Isimu na Lugha.* Dar es Salaam. Education Publishers and Distributors.

Zubeir, S. Z. (2015). *Etimolojia ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba kwa Utambulisho wa Utamaduni wa Wapemba*. Tasnifu M.A Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.